



Fifth EsF Assembly
Hyderabad, India
30 July-August 13, 2016

Montessori Education for Social Change
Serving Humanity - Celebrating Solidarity

2016 EsF Assembly Daily Summary

Monday, 8 August 2016

Lynne Lawrence alifungua wiki ya pili kwa WWM kwa nukuu toka kwa Renilde Montessori na kwa lulu ya siku. Aalimtambulisha mzungumzaji wa siku Dr Prithika Chary ambaye mama yake alihudhuria moja ya kozi zilizotolewa na Maria Montessori wakati akiwa India. Dr Chary alizungumzia juu ya maendeleo ya ubongo katika hatua ya kabla na baada ya kuzaliwa. Dr Chary alielezea uwepo wake katika tasnia ya utabibu kwa kuonyesha miujiza ya asili kwa kila mtoto. Alielezea jinsi mazingira yanavyoweza kusaidia ukuaji wa misipa ya fahamu na jinsi mambo mbalimbali kama kutelekezwa kunavyozuia ukuaji bora wa ubongo. Dr Chary alionyesha kwamba kanuni za Montessori kama kurudiarudia, mwendo na uchaguzi ni muhimu katika maendeleo ya binadamu, hususan katika miaka ya mwanzo ya utoto.

Katika chai ya asubuhi, tulifanikiwa kusheherekea siku ya kuzaliwa ya mmoja wa washiriki Matesha kutoka Tanzania kwa kuletewa Keki ya chocolate kwenye meza iliyopambwa maua na majani yeliyoandikwa jina la Matesha. leo washiriki walipata nafasi ya kuangalia na kununua vitu vya asili kama wanasesere wa mbao na baadhi ya vitabu vilivyoandikwa na mshiriki wa WWM Christinia. Lynne alishauri kwamba washiriki wote leo wataunganishwa na kiungo kiitwacho Dropbox ambapo taarifa zote zitakusanywa hapo.

Baada ya chai ya asubuhi, Lynne alimtambulisha Amukta Mahapatra ambaye ni Mkurugenzi wa shule ya Scape, kituo kwa Waelimishaji kitoacho mafunzo kwa vitendo hapo Tamil Nadu India. Amukta amefanya kazi ya kuleta usawa wa elimu katika shule za serikali. Alianzisha kama mradi mdogo bila kutarajia aina ya mafanikio. Amukta alikumbushia maendeleo ya mradi kama ulivyoandaliwa na kusambaa mataifa mbalimbali kama matokeo ya kazi nzuri ya Waziri wa Elimu.

Baada ya chakula cha mchana, Dr Prithika Chary alirudi na kuwasilisha mada ya pili juu ya vijana na kemia ya upendo. Hili lilikuwa na mtazamo wa kipekee juu ya jinsi homoni zinavyotengeneza tabia zetu. Dr Prithika pia alizungumzia juu akili ya utu uzima na kutambulisha baadhi ya vitu vya asili kutoka majikoni mwetu vinavyoweza kusaidia kuelezea sehemu hii ya uzee.

Mwisho wa siku tulimuaga Philip O'Brien. Washiriki waliweza kujiunga na wanawake wa vijijini katika kujifunza jinsi ya kutengeneza mapambo ya maua. Hii ilifuatiwa na kundi zima kusheherekea kwa ngoma wakizunguka maua katika bustani ya wazi na baadaye kufuatiwa na chakula cha jioni hapohapo nje ya bustani.